# SHIRIKISHO LA VYAMA VYA WAFANYAKAZI TANZANIA - TUCTA

## MAONI YA SHIRIKISHO KWENDA TUME YA MABORESHO YA KODI TANZANIA

## YAMEWASILISHWA NA KAMATI YA TUCTA MKOA WA DAR ES SALAAM

1. ***Sisi Wafanyakazi tuliopo Mkoa wa Dar es salaam, kwa niaba ya Wafanyakazi wengine wote Nchini, tunaomba kuondolewa kwa Kodi kwenye Posho mbali mbali kama vile posho ya nauli, posho ya chakula, posho ya nyumba, motisha ya Utendaji Bora na Posho nyinginezo***

   Katika Risala ya Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania, TUCTA Taifa kwa Mgeni Rasmi kwenye Maadhimisho ya Mei Mosi 2024 jijini Arusha, wafanyakazi walizungumzia suala hili la kuomba kuondolewa kwa Kodi katika Posho mbalimbali kama tulivyoandika hapo juu.

   Kama haitoshi katika mkutano mkuu wa TUCTA TAIFA 2024 uliofanyika jijini Dodoma mwezi Oktoba 2024, Mkutano Mkuu uliweka AZIMIO la kuomba kuondolewa kwa kodi katika posho mbali mbali kwa wafanyakazi.

   **Sababu za kuwasilisha OMBI hili ni:**

   1. Mpaka sasa kuna baadhi ya Taasisi za kiserikali ambazo Posho hizi hazikatwi kodi. Sisi wote ni wafanyakazi watanzania si vyema sana kutugawa/kutubagua katika umoja wetu.
   2. Sababu ya pili ni kuwa wafanyakazi tunalipwa hizi Posho kwa lengo la Kwenda kuzitumia kwenye mahitaji na huduma ambazo zinakatwa kodi, tena kwa mfumo mzuri uliowekwa na Serikali ikiwemo VAT na tozo mbalimbali. Hivyo basi, wafanyakazi tunakuwa wanyonge kwa kuona kuwa posho hizi zinakatwa Kodi mara mbili.
   3. Sababu ya tatu, mamlaka ya mapato imeanzisha kanuni ya kukusanya malipo yote anayoyapata mfanyakazi na kumkata kodi mwishoni mwa mwezi husika. Hii inapelekea takribani Posho zote za mfanyakazi kukatwa kodi kwa kiwango cha 30% na hivyo kushindwa kukidhi kupata huduma husika kutokana na fedha Kupungua.

2. ***Kupunguziwa Kodi katika Mshahara wa Mfanyakazi***

   Ndugu mwenyekiti wa Tume, sisi wafanyakazi tumefarijika sana kuona nia njema ya mheshimiwa Rais kuunda Tume ya Kukusanya maoni kwa ajili ya Maboresho ya Kodi.

Hapa chini tumeambatanisha namna  awamu ya NNE ya Serikali pamoja na awamu ya TANO zilivyoshughulikia maombi ya Wafanyakazi Nchini kuhusu kupunguziwa ama kupatiwa nafuu ya kodi kwa lengo kuu la kuwawezesha kujikimu wanapolitumikia Taifa.

**a. SERIKALI YA AWAMU YA NNE**

Kipindi hiki pamoja na kupunguzwa kwa kodi kwenye kima cha chini, Serikali pia ilitoa msamaha wa kodi kwa kupunguza 5% kutoka kwa kila daraja la asilimia za makato ya Kodi kadri ya ongezeko la mshahara:

Awali ilikuwa ; 35% , 30%, 25% na 20%

Baada ya punguzo ikawa : 30%, 25%, 20% na 15%.

Ndugu mwenyekiti naomba kuitaarifu Tume yako kuwa viwango hivi vya asilimia ndivyo vinavyotumika hadi sasa katika kukokotoa kodi anayolipa mfanyakazi, isipokuwa kwa kima cha chini cha asilimia 15% ambacho ndicho pekee kimekuwa kikipungua taratibu hadi kufikia 8%.

Punguzo/Nafuu ya 1% kwenye Kima cha Chini kinachokatwa kodi (Tzs 270,000 hadi Tzs 520,000) kiuhalisia ni kidogo mno maana hakizidi shilingi 2,500 kwa mwezi sawa na shilingi 30,000 pekee kwa mwaka mzima kwa ngazi zote za mishahara.

Majedwali hapa chini yanafafanua zaidi

AWALI ASILIMIA  ILIVYOKUWA                    BAADA YA PUNGUZO(SASA)

| KABLA YA MSAMAHA WA KODI | | |
|---|---|---|
| S/NO | KIWANGO | ASILIMIA |
| 1 | 270,000 - 360,000 | 20 |
| 2 | 360,000 - 540,000 | 25 |
| 3 | 540,000 - 720,000 | 30 |
| 4 | ZAIDI YA 720,000 | 35 |

| BAADA YA MSAMAHA -AWAMU YA 4 | | |
|---|---|---|
| S/NO | KIWANGO | ASILIMIA |
| 1 | 270,000 - 360,000 | 15 |
| 2 | 360,000 - 540,000 | 20 |
| 3 | 540,000 - 720,000 | 25 |
| 4 | ZAIDI YA 720,000 | 30 |

**b. SERIKALI YA AWAMU YA TANO**

Serikali katika Awamu ya Tano pamoja na kupunguza Kodi katika kima cha Chini kama ambavyo awamu karibia zote zimekuwa zikifanya lakini pia ilitoa msamaha wa kodi kwa kupanua uwiano wa kiwango cha makato. Baada ya mabadiliko hayo

kiwango cha kukatwa asilimia 30% kiliongezeka hadi 1,000,000/= kutoka 720,000/= ilivyokuwa awali. Hatua hiyo ilitoa nafuu ya 5% kwenye tofauti iliyoongezeka.

Majedwali hapa chini yanafafanua zaidi
SERIKALI YA AWAMU YA TANO

| KABLA YA VIWANGO KUBADILISHWA | | |
|---|---|---|
| S/NO | KIWANGO | ASILIMIA |
| 1 | 270,000 - 360,000 | 11 |
| 2 | 360,000 - 540,000 | 20 |
| 3 | 540,000 - 720,000 | 25 |
| 4 | ZAIDI YA 720,000 | 30 |

| BAADA YA VIWANGO KUBADILISHWA | | |
|---|---|---|
| S/NO | KIWANGO | ASILIMIA |
| 1 | 270,000 - 520,000 | 9 |
| 2 | 520,000 - 760,000 | 20 |
| 3 | 760,000 - 1000,000 | 25 |
| 4 | ZAIDI YA 1000,000 | 30 |

***Wastani (asilimia) ya makato yaliyopunguzwa awamu ya nne na Viwango hivyo vya Kodi vilivyorekebishwa Awamu ya TANO ndivyo vinavyotumika hadi sasa***

**OMBI LETU WAFANYAKAZI KWA MHESHIMIWA RAIS WA AWAMU YA SITA CHINI YA MAMA YETU DR. SAMIA SULUHU HASSAN**

Tunamuomba angalie namna ya kutupunguzia kodi kwa katumia njia mojawapo kati ya hizo mbili kadri itakavyoonekana inafaa.
Hapa chini tunaleta mapendekezo mapya ya wastani (asilimia) za makato na mabadiliko ya viwango vipya makato kwa mishahara
Katika Pendekezo letu Tunapendekeza wastani wa juu wa makato (asilimia) kuwa 25% kutoka 30
Pia kama tutatumia Viwango tunapendekeza kiwango cha chini kukatwa asilimia 30 kiwe 2,000, 000/= kutoka 1,000,000/= iliyopo kwa sasa

| PENDEKEZO LA ASILIMIA 2024 | | |
|---|---|---|
| S/NO | KIWANGO | ASILIMIA |
| 1 | 270,000 - 520,000 | 7 |
| 2 | 520,000 - 760,000 | 15 |
| 3 | 760,000 - 1000,000 | 20 |
| 4 | ZAIDI YA 1000,000 | 25 |

| PENDEKEZO LA VIWANGO 2024 | | |
|---|---|---|
| S/NO | KIWANGO | ASILIMIA |
| 1 | 370,000 - 760,000 | 7 |
| 2 | 760,000 – 1,300,000 | 20 |
| 3 | 1,300,000 – 2,000,000 | 25 |
| 4 | ZAIDI YA 2,000,000 | 30 |

## 3. NAMNA YA KUONGEZA UKUSANYAJI WA KODI NA KUIMARISHA MAPATO YA SERIKALI KUPITIA AJIRA

1. ***kudhibiti na kuratibu ajira za Wafanyakazi kutoka Nje ya nchi kwa nafasi na kazi zinazoweza kufanya na wazawa***

Ndugu Mwenyekiti wa Tume, sisi shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Mkoa wa Dar es salaam katika vikao vyetu vya kikatiba na kikanuni tuliona hatari ya kupoteza mapato mengi sana yanayotokana na kodi kwa kuruhusu wawekezaji ambao si wazawa kuwa na uhuru wa kuleta wafanyakazi wengi kutoka nje ya nchi kwa shughuli zinazofanywa na Wazawa.

Hii imefanya wawekezaji wengi kuacha kuajiri watalaamu kutoka ndani na hivyo serikali inapoteza mapato mengi sana kupitia kodi (PAYE) kwa vile wafanyakazi wageni hawatozwi kodi hiyo.

Hili limeleta matatizo yafuatayo:

a. Serikali kukosa mapato kupitia PAYE za wafanyakazi wazawa, na kama tutaalikwa kuwasilisha ana kwa ana tutaweza kuainisha Taasisi hizo ambazo zimepunguza wafanyakazi kwa kiwango kikubwa sana na nafasi hizo wamepewa wageni kutoka nje
b. Kuongezeka kwa tatizo la Ajira kutokana na nafasi hizi kuchukuliwa na wageni kutoka Nje ya nchi

Tunapendekeza Utaratibu wa awali wa kudhibiti watalaamu kutoka Nje na Kuruhusu kwa vibali maalumu kwa nafasi ambazo wazawa hawana ujuzi nazo urejeshwe ili kuondoka tatizo tajwa hapo juu

2. ***kupunguza kwa wafanyakazi wa muda (vibarua) kwa nafasi ambazo Taasisi zinahitaji watalaamu wenye ujuzi na kuajiri wafanyakazi wa kudumu***

Ndugu mwenyekiti wa tume, Taasisi nyingi sana kwa sasa hivi hasa binafsi na baadhi ya Taasisi za serikali zimeacha suala la kuajiri wafanyakazi kwa mikataba ya kudumu na badala yake zinawachukua watalaamu hao na kuwapa ajira za muda kwa kuwalipa posho ya siku,

Serikali inakosa kodi kwa kutozisimamia Taasisi hizi.

Tunaomba mamlaka za ajira nchini zifanye utafiti na kuweka mkazo kwa nafasi zinazohitaji wataalamu wa ujuzi maalumu waajiriwe wafanyakazi na siyo wataalamu hao kuchukuliwa kama vibarua

**Mwisho:**

Tunaishukuru sana Tume hii ya Maboresho ya Kodi chini ya mwenyekiti wake Balozi Ombeni Sefue kwa kututhamini na kutupa nafasi ya kuwasilisha maoni yetu.

Zaidi sana tunamshukuru Mheshimiwa Rais Dr, Samia Suluhu Hassan kwa nia yake njema ya kuunda Tume ya kukusanya maoni kwa ajili ya Maboresho ya kodi

Mwenyezi Mungu awatangulie katika kutimiza jukumu hili mhuimu kwa wananchi na Taifa kwa ujumla

Ndimi

ENG. PASCHAL LUGAGA {0763508154} KUTOKA DOWUTA

KNY: **KAMATI YA TUCTA MKOA WA DAR ES SALAAM**